www ppmedia com

# Alasiri Online

ISSN 0856 Na. 001 Jumanne January 29, 2018 Tanzani 500/- Kenya 50/-



# 'Sipendi unene'



## Darassa afunguka ubwiaji unga



## Mitanda-oni kuwaka moto






# Sipendi unene

Na Anaeli Mbise

MREMBO kutoka Bongo 'Movies' Kajala Masanja amefunguka kuwa kati ya vitu ambavyo anavichukia kwa sasa ni unene uliopitiliza

Akizungumza na Alasiri Online, amesema ubonge wake kwa sasa umefikia kiasi cha kumnyima raha kutokana na nguo nyingi kushindwa kuzivaa kwa sababu hazimtoshi.

"Jamani huu mwili mpaka nahofia naweza kupata presha au gonjwa lolote linalotokana na kunenepa sana maana hata mazoezi naona sasa yamedunda, najitahidi kupambana ili niweze kurudi kama zamani," amesema Kajala.

Msanii huyo amecheza filamu kama vile Kigodoro, House Boy, Vita Baridi, You and Me pamoja na Devils Kingdom.

# MITANDAONI KUWAKA MOTO

Na Mary Kadoke

KIAMA cha wasanii wanaotumia mitandao ya kijamii kutuma picha zao za utupu kimewadia baada ya Naibu Waziri wa Habari Sanaa na Michezo, Juliana Shonza kuahidi kuchukua hatua kwa yeyote atakayekaidi misingi iliyowekwa.

Amesisitiza hilo kupitia ukurasa wake wa Instagram @juliana_shonza, ikiwa ni siku chache tangu Rais John Magufuli atoe malalamiko juu ya watu wanaorusha picha za utupu kwenye mitandao hiyo.

"Walengwa natumai kuwa ujumbe wenu mmeshaupata kina @gigy_money_og na wenzio msidhani hatuwaoni," aliandika Shonza.

Akiongeza:"Ashupazaye shingo yake atavunjika na wala hatapata dawa."

Hivi karibuni jijini Dar es Salaam Rais Magufuli katika uzinduzi wa kifaa kitakachotumika katika mawasiliano kilichokabidhiwa kwa Mamlaka ya Udhibiti wa Mawasiliano (TCRA), aliiomba mamlaka hiyo kushughulikia watu wanaoharibu maadili kwa kutuma picha za utupu.

"Mitandao ya kijamii inaleta sana mmong'onyoko wa maadili, unakuta mtu anapiga picha ya utupu anarusha kwenye mitandao, TCRA washugulikieni wanaotumia hiyo kuharibu maadili," alisisitiza Magufuli.

# Darassa afunguka ubwiaji unga

Na Anaeli Mbise

BAABA ya kukaa kimya kwa muda mrefu mwanamuziki Darassa amefungua kwa mara ya kwanza sakata la kutumia madawa ya kulevya kwa kusema kuwa hiyo ilikuwa ni skendo iliyotengenezwa na watu.

Akizungumza na Alasiri Online, Darassa amesema kuwa stori hizo zilitengenezwa kwa lengo la kuharibu brand yake kwa kutaka kujua undani wa ukimya wake.

"Sijui ni nani na sijui alitoa wapi? hizo stori zilikuja kwa lengo la kuja kuniharibu kisaikolojia, lakini nilikuwa very positive kuzi-handle," amesema Darassa.

Darassa amesema kimya chake cha mwaka mmoja kwenye gemu, kilisababishwa na malezi ya mtoto wake na kujiandaa kimuziki zaidi ikiwemo kurekodi ngoma mpya ya Chanda Chema unaozungumzia mwanamke mrembo ambaye anafaa kuwa mke wa ndoa.

Kwa upande mwingine, Darassa amesema kuwa wakati yupo kimya wimbo pekee uliomvutia zaidi ni wimbo wa Iokote wa Maua Sama.

Darassa amekaa kimya kwa miaka miwili bila kuachia ngoma wala kufanya mahojiano na chombo chochote cha habari.



# Profesa Jay bado ndani ya gemu

**Na Anaeli Mbise**

MBUNGE wa Mikumi Joseph Haule, maarufu kama Prof Jay, ameachia ngoma mpya inayokwenda kwa jina la Woman.

Akizungumza na Alasiri Online, Prof Jay amesema kuwa ngoma hiyo inazungumzia umuhimu wa wanawake wote duniani katika kuleta maendeleo na mabadiliko chanya katika jamii pamoja na changamoto wanazopitia kila siku.

"Ni ngoma maalum kwa kuwaenzi wanawake wote Duniani na changamoto wanazopitia kila siku, lakini hawakati tamaa na mwisho wa siku wanafanikiwa," amesema Prof Jay.

Mwanamuziki huyo amemshirikisha Victoria Kimani kutoka Kenya.

Video imeongozwa na Msafiri kutoka Kwetu Studio, kwa upande wa audio ameitengeneza Abby Dady.



# Fis Q mwendo wa kobe

**Na Mary Kadoke**

**MAFANIKIO hayaji kwa kukata tamaa, kukatishwa tamaa na kila jiwe linalopondwa katika hatua za maendeleo yako ya kila siku.**
**Fid Q amesisitiza hayo kupitia ngoma yake mpya  Mafanikio  akitilia mkazo kwamba safari ni hatua na kufika inabidi kuanza mdogo mdogo.**
**Haina kusita ukiiingia lazima ukaze ingia ufuate mkia kukimbia ni mwiko kuanzia ulipo si sawa na kubakia ulipo,  amesema akinukuu moja ya mstari uliopo kwenye ngoma hiyo.**
**Akiongeza,  Nikisema chini hapana inamaana fanya unyanyuke amini umesimama komaa usianguke ukijituma na neema imekaribia achana na yasiyokuhusu.  aliongeza.**
**Ngoma hii aliyomshirikisha Baraka The Prince ina watazamaji 66,027 katika mtandao wa YouTube mpaka sasa.**
**Imetayarishwa na producer Concher na beats kuweka na  Wanene Studios akishirikiana na Chizan Brian.**
**Amewahi pia kutamba na kibao cha Sihitaji Marafiki na Ole Chiza.**

# *Amini hataki kiki*

**Na Mary Kadoke**

**WAKATI wasanii wa Bongo wakiteseka kwa kusaka kiki mitandaoni ili ziwainua kimziki, kwa Msanii Amini yeye mdogomdogo tu, amesema haitaji kiki wala purukushani za hapa na pale ili kuendelea kuwika mjini hususani kwenye suala la muziki wake.**
**Ameyasema hayo alipofanya mazungumzo na Alasiri Online na kueleza kuwa ukimya wake umekuwa wa tahadhari kulinda soko lake la muziki.**
**"Lengo langu ni kufanya mapinduzi katika kazi zangu, ni lazima kuwa makini na kufanya mambo kwa tahadhari wakati unapotoa singo,  amesema Amin.**
**Amesema yeye ni msanii mkubwa ambaye ana mashabiki wengi, hivyo kutoa nyimbo mfululizo bila kuangalia soko inaweza kumuondoa katika njia.**
**Awali miaka ya nyuma alitamba zaidi na kibao kama Robo Saa aliyoiachia 2016 na Ni Wewe 2013.**
**Kwa sasa anatamba na kibao chake cha Sijui kilichotoka mwaka jana na mpaka sasa kina watazamaji 114,000 katika mtandao wa YouTube.**
**Kiki iliyowahi kushika chati za juu ni habari ya Young Dee kutaka kufunga pingu za maisha, hata hivyo baadae iligundulika kuwa ni video baada ya kuachia ngoma yake ya Naoa siku chache baadaye.**
**Aidha wimbo huo ulikiki kwenye mitandao ya kijamii kama YouTube na Instagram baada ya kuachiwa rasmi.**

